

# Kilipo na kuchaguwa uchafu



Kila mtaa unaandaa na kuchaguwa uchafu. Kupewa pesa ya iyo kituwo inalombwa kilipo cha muji<sup>1</sup> (nafasi ya kutilia uchafu) na fatana kwa muji na lingine.

Kwa mfano, pa Liège, unapashwa lipa euros mia moja kwa mwaka kama upo mwenyewe na euros mia moja makumi tano na tano kama una jamaa.

Angalisho, iyo kilipo inanza tariki moja mwezi wa kwanza wa mwaka uyu : na kama unaama, unabaki tu na kulipa kwenye mtaa wako wazamani.

Kila jamaa inahalikwa kuchaguwa uchafu kufatana na kanuni mtaa inawapa. Kuchaguwa uchafu imelazimishwa, kama autii izo kanuni unapashwa pata matatizo za kulipa pesa

Kwa wakati mwengine, kuchaguwa uchafu inapangwa namna ifwatayo :

Mfuko wa rangi wala nafasi ya kuekeya uchafu imfanyikwa kwa kutilia uchafu wa nyumba yenye aiweze chaguliwa. Na mifuko iyo ina lokotwa kila juma kufatana na mupango yenye mtaa inawapa.



Mfuko wa rangi ingine inapangwa kwa PMC (plastiques, chuma, mfuko wa pombe) wanatupa ma vifunguo na machupa ya plastiques, mikebe ya sardine wala tomates, mikebe ya soda, aifae kutupa ingine vitu kwani wanaweza kuikatala kuichukuwa.



Mifuko inalokotwa kila mara na mupango yenye mtaa inapanga.

Angalisho, makopo, mifuko ya plastiques, kartasi ya aluminium aziko ma PMC.

Na kama unashita unaweza angalia ma sanamu na mafasiriyo yenye inachapwa ku ifuko ya PMC.



<sup>1</sup> Wenye kuwa na malipo ndogo wanaweza lombwa kutolipa.



Makartasi na vifungiyo inapashwa wekewa pembeni, wanaichaguwa na kuifunga ndani ya kituo kubwa, kartasi piya inalokotewa kila juma kwa kufatana na mupango wa mtaa.



Vitu vya kuhuziabiweze tupwa ndani ya nafasi ya kutilia uchafu. Inalokotwa mara moja kwa mwezi wala kwa namba ya simu yenye mtaa inawapa, vitu kumbwa, ma chuma, viti, vitanda, abiweze tupwa kwenye balabala mpaka siku watalikamata.



Angalisho : Vyombo zakupigia, television, video, uchafu wa majengo azilazimishwe, zinapashwa enda tiliwa kwenye kiwanda ya conteneurs.

Kilauri zinawekwa ndani ya muviringo ya vilauri yenye inapatikana kwenye balabala :

Machupa na chupa ndogo ya kilauri inatupwa wazi na safi kwa kutenga kilauri ya mweupe nay a rangi. Ndani ya miji zingine, kulokota vilauri inafanyika nyumbani.



Ndani ya mitaa zingine, wakati nalipa kilipo ya mtaa, napokea vikartasi halali ya kubadirisha na mifuko ya kutiliya uchafu. Na kama namaliza mifuko yangu, unaweza kuiuza ndani viwanda na nafasi kamili yenye zinauziswa. Ndani za mtaa zingine kunakuwa mfano wa ma conteneurs za puce. Kulipa kwangu kwa mtaa kina ni ruhusu kuwa na ruhusa ya kukamatwa kwa uchafu yangu kwa bure : kwa kupitiya iyo, ndalipa kilos zenye zinapita.

Kunakuwa namna ingine juu yakukinga uchafu ndani ya nyumba. Kiini ni kwamba kihalika watu waondowe kidogo uchafu.